

Kibali cha Mzazi/Mlezi cha Huduma za Ushauri

Mwanafunzi		Tarehe	
Mzazi / Mlezi		Gredi	
Shule			

Kibali/ruhusa yako inahitajika ili huduma zifuatazo zianze kutekelezwa kwa mwanafunzi wako:

- Huduma za matatizo ya kitabia zinaweza kujumuisha; ushauri wa kibinafsi, ushauri wa kundi na kuunda ustadi wa kijamii/kitabia. Huduma hizi zinatolewa na wafanyakazi wa Ushauri wa Shule wanaofafanuliwa kama Washauri wa Shule wenye Leseni, Wahudumu wa Jamii na Wanasaikolojia walio katika shule ya mtoto wako au wafanyakazi walio katika Idara ya Huduma za Wanafunzi ya Wilaya ya Shule za Canyons. Ikiwa mtoa huduma anapokea usimamizi wa utabibu kulingana na Idara ya Utah ya Kutoa Leseni za Kitaalamu (DOPL), taarifa zinaweza kushirikiwa kulingana na mkupuo wa mashauriano.

Kibali/ruhusa yako itadumu kwa mwaka mmoja (1) (siku 365) kuanzia tarehe ya kutia saina isipokuwa ubatilishe kibali chako kwa kuandika ambacho utawasilisha kwa mkuu wa shule au Wilaya, chochote kitatokea kwanza.

VIPENGELE VINAVYOTARAJIWA VYA MAJADILIANO

Kulingana na hali ya tatizo na hoja zinazojitokeza zilizoletwa wakati wa mahojiano ya kwanza au vikao vya ushauri na mzazi au mlezi, chini ya Sheria ya Utah ya §53E-9-203, mhudumu au wakala wa wilaya ya shule kimsingi wanapaswa, isipokuwa katika hali chache, kupata ridhaa yako kama mzazi au mlezi wa kisheria ili kujadili ikiwa taarifa zitahitajika kutoka kwa mtoto wako kuhusu masuala yafuatayo:

- a) misimamo ya kisiasa au, isipokuwa kama ilivyotolewa chini ya Sheria ya Utah § 53G-10-202 au kanuni za Bodi ya Elimu ya Jimbo, filofilia za kisiasa
- b) matatizo ya kiakili au ya kisaikolojia
- c) tabia za kingono, uelekeo au fikra
- d) tabia mbaya, isiopatana na watu, ya kujilaumu, au ya kudhalilisha
- e) kuwakosoa watu ambao mwanafunzi au mwanafamilia ana mahusiano ya karibu ya kifamilia
- f) mahusiano au imani za kidini
- g) faida na mahusiano yanayotambuliwa kisheria, kama yale ya mawakili, wafanyakazi wa tiba, au wabunge
- h) mapato, isipokuwa kama inavyohitajika kisheria

KIPINDI CHA KUSUBIRI IDHINI

Maelezo yaliyokusanywa katika mahojiano haya yatatumiwa kuunda mpango wa matibabu. Maelezo yaliyokusanywa wakati wa kipindi hiki cha ushauri yatajumuishwa katika mpango wa matibabu. Sheria inayotumika inahitaji muda wa kusubiri wa wiki mbili kabla ya mwanafunzi kuhojiwa kuhusu masomo haya, isipokuwa mzazi aondoe muda huu wa arifa. Saina yako itaturuhusu kuondoa muda wa kusubiri na kutoa huduma kwa mtoto wako mara moja.

TAARIFA ZINAZOHITAJIKA

Watoa huduma wana jukumu la kuhakikisha kwamba msimamizi anayefaa amefahamishwa kuhusu maelezo yoyote ambayo yanahusu matatizo yanayotarajiwa au hali za hatari ambazo zinaweza kutokea. Iwapo mfanyakazi au wakala wa shule anaamini kuwa kuna hali inayoleta tishio kubwa kwa ustawi wa mwanafunzi, mfanyakazi au wakala huyo atamwarifu mzazi au mlezi wa mwanafunzi bila kuchelewa. Maelezo yaliyokusanywa kutoka kwa vikao vya mahojiano au ushauri yanaweza kushirikiwa na msimamizi au mhudumu mwingine wa shule kwa msingi wa hitaji-la-kujua pekee. Maelezo kuhusu mwanafunzi kutumia dawa au pombe yataripotiwa kwa wazazi. Sheria za Jimbo zinahitaji kwamba lazima maelezo yanayoonyesha dhulumu kwa watoto yariptiwe kwa shirika linalofaa la kiserikali (Sheria ya Utah §53G-9-209).

Uwasilishaji wa Huduma kwa Mbali: Huenda hali fulani zikahitaji huduma zitolewe kwa mbali. Huduma zinazotolewa kwa mbali kimsini si salama na sio za siri zikilinganishwa na huduma za ana kwa ana.

- Wakati wa huduma za mbali za ana kwa ana, wewe au mtu mwingine katika kaya anaweza kutazama kipindi, kuona au kusikia maelezo ambayo yanakusudiwa kuwa ya siri.
- Wakati wa huduma za mbali za kikundi, wewe au mtu mwingine katika kaya anaweza kutazama kipindi, kuona au kusikia maelezo kuhusu mwanafunzi wako au watu wengine ambayo yanakusudiwa kuwa ya siri. Watu katika maeneo mengine pia wanaweza kuona au kusikia maelezo kuhusu mwanafunzi wako ambayo yanapaswa kuwa ya siri.

Wazazi ambao wangependa maelezo ya ziada wanaweza kuwasiliana na msimamizi wa shule aidha kabla au baada ya huduma kutolewa.

Ninaruhusu mtoto wangu ashiriki katika vikao vya ushauri na kuondoa kipindi cha kusubiri cha wiki mbili ili huduma zianze mara moja. Ikitokea haja, mtoto wangu anaweza kujadili masuala yaliyotajwa hapo juu wakati anapokea huduma za ushauri.

Jina Lילוandikwa la Mzazi/Mlezi		Tarehe	
Saina ya Mzazi/Mlezi		Uhusiano na Mwanafunzi	

Iwapo utahitaji maelezo zaidi, au una maswali au wasiwasi, tafadhali piga simu kwa: